SHERIA YA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA
NAM.2 YA MWAKA 2007

# KANUNI ZA MALIPO, ADA NA HUDUMA 2014

ZANZIBAR

JULAI, 2014

SHERIA YA KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

NAM 2 YA MWAKA 2007

KANUNI ZA MALIPO, ADA NA HUDUMA

(Chini ya kifungu cha 67(2))

KWA UWEZO niliopewa chni ya kifungu cha 67 (2) cha Sheria ya Kamisheni ya Wakfu Na Mali ya Amana, Nam,2 ya mwaka 2007. Mimi ABUBAKAR KHAMIS BAKARY, Waziri wa Katiba na Sheria Zanzibar, natunga kanuni zifuatazo:

Jina fupi na kuanza kutumika

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Malipo, Ada na Huduma 2014 na zitaanza Kutumika mara tu baada ya kusainiwa na Waziri.

Ufafanuzi

2. Katika kanuni hizi isipokuwa maelezo yakihitaji vyenginevyo:

"Gazeti" maana yake ni Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Kamisheni" maana yake ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Katibu Mtendaji kama ilivyofafanuliwa chini ya kifungu cha 9 cha Sheria.

"Mali ya Amana" maana yake ni kama ilivyofafanuliwa kwenye Sheria.

"Mali ya Wakfu" maana yake ni kama ilivyofafanuliwa kwenye Sheria.

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Nam. 2 ya mwaka 2007 pamoja na marekebisho yake.

"Waziri" maana yake ni Waziri anayesimamia masuala ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana.

Chanzo cha mapato

3. Fedha na vyanzo vya mapato ya Kamisheni vitakuwa:

(a) Malipo na ada mbali mbali zinazokusanywa na Kamisheni.

(b) Malipo yote au mali inayolipwa Kamisheni kuhusiana na jambo

lolote linaloambatana na kazi zake.

(c) Ruzuku, michango, wasia au msaada mwengine wowote ulitolewa kwa Kamisheni.

(d) Miradi mbalimbali kama itakavyoanzishwa na Kamisheni.

Huduma kutototolewa bure

4. Hakutakuwa na huduma yoyote itakayotolewa na Kamisheni bila ya malipo isipokuwa ile iliyotajwa na Sheria au kanuni.

Malipo kuhusu urithi

5. Kutakuwa na malipo ya ushuru wa malimaiti (estate duty) ambayo yatatozwa kwa asilimia zero nukta mbili tano (0.25%) ya mali yote inayotaka kurithiwa.

Malipo ya urithi kutopewa kipaumbele

6. Malipo yaliyotajwa katika kanuni ya 5 ya kununi hizi yatakatwa baada ya kutolewa madeni yote ya marehemu na wasia kama upo.

Ada nyenginezo kuhusu urithi

7. Ada nyengine zinazohusu urithi zitatozwa na kulipwa kwa mambo mbali mbali yaliyoorodhehwa kwenye Jadweli la kanuni hizi na malipo hayo yanaweza kutozwa katika fedha zozote zilizopokelewa na Kamisheni.

Malipo kuhusu wakfu na amana

8(1) - Kutakuwa na malipo ya ujira wa wakfu unaotokana na kodi ya mali ya wakfu ambayo yatatozwa asilimia kumi (10%) ya kodi hiyo.

(2)- Kutakuwa na malipo ya ujira wa dhamana ya amana unaotokana na kodi ya mali ya amana au malipo ya amana nyenginezo, ambayo yote hayo kila moja yatatozwa asilimia kumi (10%) ya pato lake.

(3) - Kutakuwa na malipo ya ujira wa dhamana ya mayatima unaotokana na kodi ya mali ya amana kwa mayatima.

Ada nyenginezo kuhusu wakfu na amana

9. Ada nyengine zinazohusu wakfu au amana zitatozwa na kulipwa kwa mambo mbali mbali yaliyoorodheshwa kwenye Jaduweli la kanuni hizi.

Shughuli za dini na sheria

10. Kutakuwa na utozaji wa ada za huduma mbali mbali za kidini na

za kisheria kama zilivyotajwa kwenye Jaduweli la kanuni hizi.

Huduma za binafsi

11. Pale ambapo kuna mzozo au bila ya mzozo na ikatakiwa Kamisheni kuingilia kati kwa ajili ya usuluhishi wa mali yoyote ambayo haisimamiwi wala kuendeshwa na Kamisheni, basi Kamisheni inaweza kubeba jukumu hilo kwa kufatwa taratibu maalumu.

Taratibu za huduma za binafsi

12. Bila ya kuathiri maelezo yoyote ya kanuni ya 12 ya kanuni hizi, Kamisheni inaweza kubeba jukumu la usuluhishi au ufuatiliaji au mwenendo mwengine wowote unaofaa kisheria wa mali ya watuau taasisi yoyote pale wadai husika watakapokamilisha mambo yafuatayo:

(a) Wadai kuwasilisha kimaandishi ombi maalumu kwa Kamisheni.

(b) Kulipia gharama zote za usafiri na kujikimu kwa kipindi chote cha safari ya eneo husika.

(c) Kulipa posho kwa maafisa wa Kamisheni na watendaji wengine wowote wataohusika katika shauri hilo.

(d) Kulipa dhamana ya huduma binafsi kama ilivyotajwa kwenye Jaduweli.

Malipo kulipwa baada kukubaliwa ombi

13. Ada na malipo yote yaliyotajwa kwenye kanuni ya 13 ya kanuni hizi hayatolipwa ili baada ya kukubaliwa ombi la huduma biafsi na Katibu Mtendaji.

Kushindwa kulipa ada,huduma au malipo mbalimbali

14. Pale ambapo mtu atashindwa kulipia gharama, ada au malipo yoyote yaliyotajwa kwenye kanuni hizi hatostahiki kupatiwa huduma yoyote anayoihitajia.

Kushindwa kulipia kwa sababu za umaskini n.k

16(1)- Pale ambapo mtu atashindwa kulipia gharama, ada au malipo yoyote yale yaliyotajwa kwenye Kanuni hizi kwa sababu za umasikini au sababu nyenginezo atalazimika kufuata utaratibu ufuatao:

(a) Kujieleza vya kutosha na kuthibitisha kwa maandishi hadi Katibu Mtendaji aridhike juu ya kushindwa kwake kulipia huduma anayoihitajia.

(b) Kutiiagizo, amri au masharti yoyote atakayopewa na Kamisheni kuhusiana na huduma anayoihitajia.

(2)- Katibu Mtendaji akiridhika anaweza kuruhusu kutolewa bila ya malipo huduma Iliyoombwa kwa masharti au bila masharti yoyote.

(3) Mtu asiporidhika na maamuzi ya Katibu Mtendaji anaweza kuomba shufaa ya Waziri ambae maamuzi yake yatakuwa ya mwisho.

(4)- Maelezo ya para ya (1), na (2) ya kanuni hii hayatahusika na kanuni ya 5 na ya 8 ya Kanuni hizi.

Kukosekana kwa kanuni

17(1)- Kukosekana kwa kanuni yamalipo juu ya huduma yoyote inayotolewa na Kamisheni Haikuizuii Kamisheni kudai malipo ya huduma hiyo kwa kuzingatia kanuni ya 4 ya Kanuni hizi.

(2)- Malipo yatakayotozwa chini ya para ya (1) ya kanuni hii yataamuliwa na Katibu Mtendaji baada ya kushauriana na Mhasibu Mkuu au Afisa mwengine yeyote Anayehusika na huduma hiyo.

Marekebisho

18. Waziri kwa kutangaza kwenye Gazeti Rasmi anaweza kurekebisha ama kubadilisha Kanuni yoyote au Jaduweli au ada yoyote iliyotajwa kwenye kanuni hizi pindi akiona kuna haja ya kufanya hivyo.

IMETIWA saini leo tarehe .................... mwezi wa ............................ 2014

..................................................

ABUBAKAR KHAMIS BAKARY
Waziri wa Katiba na Sheria
ZANZIBAR

**JADUWELI**

| NAM. | HUDUMA | MALIPO |
|---|---|---|
| 1. | Ujira wa usimamizi wa Wakfu | 10% |
| 2. | Ujira wa dhamana ya amana | 10% |
| 3. | Ujira wa dhamana ya Mayatima | 5% |
| 4. | Usajili wa wakfu | 10,000/- |
| 5. | Mkataba wa upangaji | 10,000/- |
| 6. | Fomu ya kufungulia mirathi | 2,000/- |
| 7. | Kutafutiwa kumbukumbu | 5,000/- |
| 8. | Kutafutiwa kumbukumbu idara ya nyaraka | 10,000/- |
| 9. | Hati ya kiapo | 5,000/- |
| 10. | Hati ya uwakala | 5,000/- |
| 11. | Fomu na kujaziwa waraka | 10,000/- |
| 12. | Kopi ya maamuzi ya mahakama au mwenendo wa shauri | 10,000/- |
| 13. | Cheki iliyomaliza muda | 2,000/- |
| 14. | Kufuta amana | 20,000/- |
| 15. | Utafiti kwa wakaazi wa Zanzibar | 50,000/- |
| 16. | Utafiti kwa wageni (baada ya kupata ruhusa mamlaka husika) | 50$ |
| 17. | Tazkiya | 3,000/- |
| 18. | Kujaziwa fomu ya ithibati | 3,000/- |
| 19. | Ombi la msamaha wa ushuru wa forodha | 1% |
| 20. | Hati ya usajili wa taasisi | 100,000/- |
| 21. | Tafsiri kila ukurasa | 10,000/- |
| 22. | Barua ya uwakala | 10,000/- |
| 23. | Barua ya Usimamizi wa Mirathi | 10,000/- |